**MPANGOKAZI WA UTEKELEZAJI ULIOASILIWA (ADOPTED) NA WAZIRI WA NCHI OR-TAMISEMI (MHE.GEORGE B. SIMBACHAWENE [MB]) KUTOKA RISALA YA WAGANGA WAKUU WA MIKOA NA HALMASHAURI, MWAKA 2017**

| Na | Hoja | Shughuli/Utekelezaji | Muda wa utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Upungufu wa watumishi wa asilimia 49.5% unaopelekea vituo 285 kuongozwa na wahudumu wa afya, vituo 1505 kuongozwa na wauguzi. Upungufu huu ni uliotokana na upungufu uliokuwepo pamoja na upungufu uliotokana na vyeti vya kughushi | Kuajiri watumishi 7304 katika mwaka wa fedha 2017/18 ili kupunguza upungufu uliopo. Kwa kuanzia, watumishi 3439 waajiriwe kuziba pengo la watumishi walioondolewa kwenye utumishi kwa sababu ya vyeti vya kughushi, kabla au ifikapo Septemba 2017 | Julai-Septemba 2017 | OR-TAMISEMI |
| | | Kuajiri watumishi wengine wa sekta ya afya 3865 kupunguza upungufu ifikapo Juni 2018 | Julai 2017-Juni 2018 | OR-TAMISEMI |
| 2 | Utekelezaji usioridhisha wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) ambao unaelekeza kila kijiji kuwa na zahanati na kila kata kuwa na kituo cha afya, ambapo mpaka sasa vijiji 7991 havina zahanati na kata 3910 hazina vituo vya afya | OR-TAMISEMI itoe maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri, Kila Halmashauri ijenge kwa ukamilifu angalau zahanati mbili (2), na vituo vya afya viwili (2) tu kwa kila mwaka (Jengo la OPD na RCH na nyumba angalu 3 za watumishi (two in one) pamoja na vichomea taka katika vijiji/maeneo ambayo ni kipaumbele | Julai 2017 | OR-TAMISEMI |
| | | Kila Halmashauri ijenge kwa ukamilifu angalau zahanati mbili (2), na vituo vya afya viwili (2) tu kwa kila mwaka (Jengo la OPD na RCH na nyumba angalu 3 za watumishi (two in one) pamoja na vichomea taka katika vijiji/maeneo ambayo ni kipaumbele | Kila mwaka wa fedha | Wakurugenzi wa MSM |
| | | Kuwe na Sera ya Kila kijiji/Kata kuwa na Zahanati/Kituo cha Afya vilivyokamilika kama sharti la kusajiliwa kuwa kijiji au kata | Mwaka wa fedha 2018/19 | OR-TAMISEMI |
| 3 | Uwepo wa maboma 1,580 ambayo hayajakamilika yanayojumuisha majengo ya vituo na nyumba za watumishi. | OR-TAMISEMI itoe maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri, kutumia asilimia 40% ya fedha za miradi ya Maendeleo (LGCDG) kukamilisha maboma ambayo hayajakamilika | Kabla au kufikia tarehe 14 Julai 2017 | OR-TAMISEMI |
| | | MSM kutumia asilimia 40% ya fedha za miradi ya Maendeleo (LGCDG) kukamilisha maboma ambayo hayajakamilika | Kila mwaka wa fedha, mpaka maboma yote yaliyopo kuwa yamekamilika | Wakurugenzi wa MSM |
| 4 | Uwepo wa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyochakaa na visivyo na viwango (majengo madogo) | Kuwepo na Mfuko maalumu wa uboreshaji Miundombinu ya Afya (Health Facility Infrastructure fund) kama ilivyo kwenye miundombinu ya Barabara | Mwaka wa fedha 2018/19 | OR-TAMISEMI |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mradi wa Malipo kwa ufanisi (RBF) utekelezwe nchi nzima | Septemba 2017 | OR-TAMISEMI |
| 5 | Uwezo mdogo wa MSD kutosheleza mahitaji halisi ya vituo (Order Fulfillment Rate) ambapo kwa sasa upatikanaji ni 30-40% | MSD iongeze ufanisi ili kuweza kutosheleza mahitaji ya vituo (Order Fulfillment Rate) kufikia 100% | Desemba 2017 | MSD |
| | | Utaratibu wa washitiri uliopo kwenye mikoa ya Morogoro, Dodoma, na Shinyanga uenezwe nchi nzima | Desemba 2017 | OR-TAMISEMI |
| 6 | Kutokuwepo kwa viwanda vya dawa na vifaa tiba nchini ambavyo vinaweza kutumia malighafi zilizopo nchini; hivyo kupelekea serikali kuagiza dawa na vifaa tiba nje ya nchi kwa gharama kubwa | Serikali itafute wawekezaji wanaoweza kujenga viwanda nchini kwa kutumia malighafi zilizopo | Juni 2018 | OR-TAMISEMI |
| 7 | Kiwango kidogo cha wananchi wanaotumia Bima za Afya (30%) sambamba na kiwango kikubwa cha misamaha (49-60%) | Muswada wa Bima kwa kila mwananchi ukamilishwe na uwasilishwe katika kikao cha Bunge lijalo | Novemba 2017 | WAMJWW |
| | | Utaratibu wa CHF iliyoboreshwa unaotekelezwa mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Arusha, utekelezwe nchi nzima | Desemba 2017 | WAMJWW |
| 8 | Fedha za OC zinazotolewa kwa ajili ya Afya kuingizwa kwenye akaunti za OC za Halmashauri, hali inayopelekea fedha hizo kutumika kwa matumizi mengine | Wizara ya Fedha ielekeze fedha za OC afya kwenye akaunti za Sekta ya Afya moja kwa moja | Kabla au kufikia tarehe 14 Julai 2017 | Wizara ya Fedha |
| 9 | Kutokuwepo miundombinu na wataalamu inayokidhi/wanaokidhi hadhi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa | Serikali itenge fedha maalum kwa ajili ya kuimarisha miundombinu (Majengo, vifaatiba kama vile MRI, CT Scan, digital X-ray, Echo) na upatikanaji wa madaktari bingwa wa nyanja zote | Julai 2017-Juni 2018 | OR-TAMISEMI |
| 10 | Kutopungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto | Ujenzi na ukarabati miundombinu ya vituo vya afya 145 uharakishwe | Juni 2018 | OR-TAMISEMI |
| | | Kutoa mafunzo na kuajiri watoa huduma wa kada zinazohitajika kwenye huduma za dharura za uzazi na watoto wachanga (CEMonC) | Juni 2018 | OR-TAMISEMI |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11 | Kutokufahamika kwa mwongozo wa JAST (Joint Assistance Strategy Tanzania) kwa watendaji ngazi za Wizara, Mikoa na Halmashauri inayosababisha uratibu usio mzuri wa wadau mbalimbali | Mwongozo wa JAST (Joint Aids Strategy Tanzania) ufafanuliwe na usambazwe kwa watendaji ngazi za Wizara, Mikoa na Halmashauri | Desemba 2017 | WAMJWW |
| 12 | Kuwepo kwa mwongozo wa uchangiaji huduma wa mwaka 1997 ambao umepitwa na wakati na ambao haukidhi mahitaji ya sasa | Mwongozo wa Cost sharing urekebishwe ili ukidhi mahitaji ya sasa | Desemba 2017 | WAMJWW |
| 13 | Uandaaji wa mpango wa CCHP kutumia muda mrefu kukamilika na mabadiliko ya mara kwa mara ya PlanRep tool | Mfumo wa web based planrep ya afya ngazi za vituo vyote zikiwemo hospitali za mikoa, CHMT, na RHMT ukamilishwe | Septemba 2017 | OR-TAMISEMI |
| | | Mikoa na Halmashauri wajengewe uwezo kwenye mfumo wa Web-Based Planrep | Septemba 2017 | OR-TAMISEMI |
| | | Mwongozo wa CCHP upitiwe upya ili kuendana na mabadiliko ya DHFF | Septemba 2017 | OR-TAMISEMI |
| 14 | Kuwepo kwa mifumo mingi ya takwimu ambayo haiingiliani na hivyo kuleta changamoto ukizingatia uhaba wa watumishi | Kuwe na Mfumo mmoja tu unaosomana wa ukusanyaji wa takwimu katika ngazi za vituo vya utoaji huduma | Juni 2018 | WAMJW/ OR-TAMISEMI |
| 15 | Kutodhibitiwa magonjwa ya milipuko kama kipindupindu katika maeneo mbalimbali hapa nchini | Halmashauri zihakikishe kila kaya zinakuwa na vyoo bora na kuvitumia, na taarifa zitolewe kila robo mwaka katika ngazi zote | Julai 2017-Juni 2018 | MSM |
| | | Halmashauri zihakikishe zinatenga maeneo ya dampo na machinjio | Julai 2017-Juni 2018 | MSM |
| | | Kuhakikisha mkakati mtambuka wa kuboresha miundombinu ya maji safi, maji taka kwa kuunda kamati tendaji zinazohusisha sekta muhimu kama afya, maji , miundombinu, ardhi, mipangomiji | Desemba 2017 | MSM |

WAANDAAJI
DKT.SAMWEL L. NHIGA - RMO SONGWE
DKT. CHARLES MICHAEL MTABHO- TMOH BABATI
DKT. SUNGWA N. KABISSI- RMO MANYARA
DKT. OBERLIN KISANGA- WAMJWW
DKT. MUSELETA NYAKIROTO- MOI/C IRINGA RRH
DKT. ATHUMAN PEMBE- OR-TAMISEMI